

**HOTUBA YA KATIBU MKUU, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA UZINDUZI
WA BODI YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO TAREHE 25
NOVEMBA, 2022 KATIKA UKUMBI WA OFISI ZA MAMLAKA YA
SERIKALI MTANDAO, JENGO LA UTUMISHI, JIJINI DAR ES SALAAM**

Mheshimiwa Jenista Mhagama (MB): Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Dkt. Mussa Muhiddin Kissaka; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya

Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Wajumbe wa Bodi; Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Eng. Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Menejimenti ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),

Wanahabari,

Mabibi na Mabwana;

NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mheshimiwa Waziri,

Awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku hii ya leo salama. Aidha, nikushukuru wewe kipekee kwa kukubali kujumuika nasi kwenye uzinduzi wa Bodi ya Wakurungezi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Bodi ambayo ni muhimu

kwa ustawii wa Taifa hususani katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Mheshimiwa Waziri,

Napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kuteua Wajumbe nane wa Bodi kwa kuzingatia vigezo vya weledi na uadilifu, baada ya Mwenyekiti wa Bodi hii kuteuliwa na Rais Wa Jamhuri wa Muungano ya Tanzania, **Mheshimiwa** Samia Suluhu Hassan. Bodi hii ina jukumu kisheria kukushauri kuhusiana na Mipango ya Serikali Mtandao, ambayo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni msimamizi wa utekelezaji wake. Hii inatokana na dhamana ya Wizara hii iliyopewa ya kusimamia Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Waziri,

Utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao ni moja ya maeneo muhimu ya maboresho yaliyofanyika katika Utumishi wa Umma, ambao umesaidia kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa Umma. Hiki ni kiwezeshi na kichocheo muhimu cha kulifanya Taifa kufikia uchumi wa Kidijitali, kushiriki kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4th Industrial Revolution) na kufikia Dira ya Taifa ya Mwaka 2025. Ili kuyafikia hayo, Bodi hii itasimamia Utekelezaji wa Sera zinazohusu Serikali Mtandao, ikiwa ni pamoja na kuthibitisha wafanyakazi wanaohusika na Uongozi wa Mamlaka.

Mheshimiwa Waziri,

Tunaamini kuwa Bodi inakwenda kuchagiza na kuongeza kasi katika utekelezaji wa jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao, zilizokwisha kutekelezwa na zitakazotekelawa, kutokana na uwepo wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Serikali Mtandao. Utekelezaji wa jitihada

za Serikali Mtandao katika taasisi za umma umeleta mafaniko mengi, ikiwemo ujenzi na matumizi ya mifumo na miundombinu mbalimbali ya Serikali Mtandao, ambayo imekuwa mhimili muhimu katika kurahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma. Kwa muktadha huo, niitake Bodi kuchukua hatua kali kwa Taasisi zinazokiuka Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa *Waziri*,

Wizara, katika kuhakikisha utekelezaji wa Serikali Mtandao unafanyika kwa usahihi, usalama na kwa kuzingatia miongozo ya Kisera, imeandaa Mkakati wa Serikali Mtandao (e-Government Strategy 2022) na Mkakati wa Serikali wa Kuzuia/Kukabiliana na Uhaliu wa Kimtandao (Government Cyber Security Strategy 2022) ili kuweka dira mahususi katika kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao, ninaielekeza Bodi hii kuhakikisha nyaraka hizi zinazingatiwa ipasavyo ili tuweze kufikia malengo tarajiwa ya kuwa na matumizi sahihi ya Serikali Mtandao, na hatimaye kuboresha utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma kwa umma.

Mheshimiwa *Waziri*,

Kwa mwaka mzima, pamoja na nafasi yangu kama Katibu Mkuu, nilikuwa Bodi kwa Mujibu wa Sheria, kupitia nafasi hiyo nimeshuhudia mafanikio makubwa yakipatikana. Hata hivyo, sambamba na mafanikio hayo, bado kuna changamoto za baadhi ya Taasisi za Umma kutozingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyoidhinishwa.

Na kwa nyakati tofauti, Ofisi yangu imekuwa ikitoa maelekezo kadhaa kwa Taasisi za Umma ikiwemo kuzitaka Taasisi zote za Umma kutumia Mfumo wa Serikali wa Ubudilishanaji Taarifa (Government Enterprise

Service Bus- GovESB) zinapohitaji kubadilishana taarifa au kupata idhini ya Mamlaka ya Serikali Mtandao kabla ya kuanzisha Mifumo ya TEHAMA. Kwa mukhtadha huo, naikumbusha Bodi unayoizindua leo kuweka msisitizo mkubwa katika kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa *Waziri*,

Baada ya kusema hayo machache, naomba nitumie fursa hii kukukaribisha ili uzungumze na hadhira hii na kisha kuizindua rasmi Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora